



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU PINGAMIZI DHIDI YA  
WAGOMBEA WA KITI CHA RAIS KWA UCHAGUZI MKUU WA  
MWAKA 2020**

Leo tarehe 26 Agosti 2020 Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea pingamizi kutoka kwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu mgombea wa kiti cha Rais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) dhidi ya Profesa Ibrahim Haruna Lipumba mgombea wa kiti cha Rais kupitia Chama cha Wananchi (CUF) na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli mgombea wa kiti cha Rais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 39(5) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, baada ya kupokea pingamizi dhidi ya wagombea hao, imewataarifu wawekewa pingamizi mapema iwezekanavyo (*with the least possible delay*) na wahusika wamewasilisha utetezi wao.

**1. PINGAMIZI DHIDI YA MGOMBEA WA CUF**

*Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria.*

Tume baada ya kupitia sababu ya pingamizi pamoja na utetezi uliotolewa imejiridhisha kuwa **Profesa Ibrahim Haruna Lipumba** amerejesha fomu zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imejiridhisha kwamba pingamizi hilo halina msingi wa kisheria na imelitupilia mbali. Kwa maana hiyo, **Profesa Ibrahim Haruna Lipumba** anaendelea kuwa mgombea halali wa kiti cha Rais kupitia Chama Cha Wananchi (CUF).

## 2. PINGAMIZI DHIDI YA MGOMBEA WA CCM

- (i) *Hakuambatisha picha kwenye fomu ya uteuzi.*
- (ii) *Hakurudisha fomu ya uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria.*

Tume baada ya kupitia sababu za pingamizi zote mbili pamoja na utetezi uliotolewa imejiridhisha kuwa **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** mgombea wa kiti cha Rais kupitia Chama Chama Mapinduzi (CCM) amerejesha fomu zake ambazo zimeambatishwa pamoja na picha kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imejiridhisha kwamba pingamizi hizo hazina msingi wa kisheria na imezitupilia mbali. Kwa maana hiyo, **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** anaendelea kuwa mgombea halali wa kiti cha Rais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kwa mujibu wa kanuni ya 39(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, sababu za uamuzi huu wa Tume watapewa kwa maandishi aliyeweka na wale waliowekewa pingamizi.

Kwa msingi wa uamuzi huu, vyama vya siasa vinavyoshiriki Uchaguzi Mkuu kwa kiti cha Rais na Makamu wa Rais vinabaki kuwa kumi na tano.

Imetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.



Dkt. Wilson M. Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

26 Agosti, 2020